

KUZITAMBUA JUMUIYA KAMA WAFANYA MAAMUZI!

Mradi wa Kituo cha Kuzalisha Umeme wa Jotoardhi cha Akiira 1 nchini Kenya

Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) inaandaa mkopo wa

€155,000,000

(Dola milioni 192) kwa ajili ya mradi wa uzalishaji **Kituo cha Kuzalisha Umeme wa Jotoardhi cha Akiira 1**

Mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa jotoardhi chenye uwezo wa


70 megawati

nje ya mji wa Naivasha, Kenya na kando ya Mradi wa Kituo cha Kuzalisha Umeme wa Jotoardhi cha Olkaria. Mradi huu unakadiriwa kugharimu

€310,000,000

(Dola milioni 380)

Mradi huu utatekelezwa na kampuni ya **Akiira Geothermal Limited**.



62.5%

ya hisa iliyobaki inamilikiwa na makampuni ya Marekani, Ram Energy na Marine Power, na kampuni ya Denmark, Frontier Markets.

Faida kwa mujibu wa Kampuni



Kutoa nishati mbadala ili kuziba pengo lililopo kati ya uhitaji na ugavi tarajiwa nchini Kenya



Kuchangia katika kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.



Kuchangia katika kupunguza umaskini na ukuaji jumuiishi wa uchumi kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za nishati ya bei nafuu, zinazoaminika, endelevu na za kisasa.

Uwezekano wa Athari kwa Jumuiya



Kupoteza ardhi



Kupoteza kipato kwa wafugaji



Uwezekano wa jamii mahalia kutofaidika moja kwa moja na mradi huu



Athari kwa mazingira, makao ya asili na wanyamapori



Kupoteza makazi

Nukuu



"Sikuhi ni salama kueleza mawazo yangu kuhusu mradi huu kwa sababu niliogopa ya kuwa kama watu hawa (maafisa wa kampuni) wangukuja hapa, pengine ningetiwa mbaroni kwa kutoa malala miko."

"Jumuiya yetu haijachukuliwa kama sehemu ya jumuiya zilizoathiriwa. Tumesahuliwa katika uwakilishi wa kamati na majadiliano yoyote yanayohu sisha jumuiya husika na kampuni hii licha ya kijiji chetu kuwa ndani ya eneo lililoathiriwa na mradi."

"Hatukushirikishwa ile Tathmi ni ya Kimazingira na ya Kijamii. Kile tukijuacho ni kupitia gumzo mtaani. Tunataka tushirikishwe taarifa hizi."

"Kampuni hii inapaswa kutupa maelezo zaidi kuhusu mradi huu; kwa sasa hatushirikishwi kikamilifu katika mchakato wa mradi huu."

"Tunataka kuungwa mkono na serikali, na kampuni hii inapaswa kuacha kuwatendea watu kwa namna isiyofaa."



"Tunataka kampuni isikilize malalamiko yetu."




TAKWIMU

Shirika la International Accountability Project na Kikundi cha Maendeleo cha Jumuiya ya Narasha (Narasha Community Development Group) walifanya utafiti kwa wanajumuiya 350 kuhusu uelewa wao wa mradi huu pamoja na mapendekezo yao kwa wafanya maamuzi.


Hivi ndivyo walivyosema:




Hawakujua ni nani atakayeteteleza mradi huu



hawakujua ni wapi pa kutoa malalamiko



HATUA ZIJAZO



Kwa kutumia matokeo ya utafiti huu, jumuiya zin aiomba serikali ya Kenya na Kampuni ya Akiira Geothermal kuheshimu haki zao za kizawa, kuwashirikisha kama wafanya maamuzi katika mchakato wa ubuni wa mradi na kushughulikia wasiwasi wao kuhusu uwezekano wa kupoteza ardhi, makazi, kipato na madhara kwa mazingira.